

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO -

TAALUMA



MAHAFALI YA ISHIRINI YA MUHAS

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) Prof. David Mwakyusa atawatunukia diploma na digrii mbalimbali wahitimu wa MUHAS, katika Mahafali ya Ishirini yatakayofanyika Alhamis tarehe **03 Desemba 2026** kuanzia saa **tatu asubuhi** katika Kampasi ya Muhimbili.

Wahitimu wote waliofaulu mitihani yao MUHAS na wanastahili kutunukiwa diploma na digrii mbalimbali na wamepanga kuhudhuria mahafali wanakumbushwa:

- Kulipia TZS 42,000 kama gharama ya kukodisha joho la mahafali kwa kuingia kwenye tovuti ya MUHAS (www.muhas.ac.tz) ili uweze kupata muongozo wa jinsi ya kulipia.
- Kufika Chuoni kwa ajili ya kuchukua joho la mahafali siku ya **Jumatatu tarehe 30 Novemba** hadi **Jumatano tarehe 02 Desemba 2026**. Majoho yatachukuliwa kwenye ofisi za Skuli na Taasisi husika kuanzia **saa 4 asubuhi mpaka saa 10 jioni**.
- Kufika Chuoni kwa ajili ya mazoezi na Wakuu wao wa Skuli na Taasisi siku ya **Jumatano tarehe 02 Desemba 2026 saa 2:30 Asubuhi** bila kukosa (**wahitimu wote ambao hawatahudhuria mazoezi haya hawataruhusiwa kushiriki kwenye mahafali**). Wageni waalikwa, wahitimu pamoja na ndugu na marafiki wa wahitimu wanaombwa wawe wameketi kwenye nafasi zao ifikapo **saa 3:30 asubuhi siku ya Alhamis 03 Desemba 2026**

Sherehe za Mahafali zitatanguliwa na sherehe za kuwapa zawadi wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma kwa mwaka **2025/2026 (Prize Giving Ceremony)** siku ya **Jumatano tarehe 02 Desemba 2026 saa 8:00 mchana**.

Prof. Emmanuel Balandya

NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – TAALUMA

